**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 18 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022:**

Ripoti ya Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

151. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika hatua za Serikali kupunguza mrundikano wa mahabusu magerezani alieleza kuwepo kwa mifumo mizuri na ya kisasa ya uchunguzi hasa kwa makosa ya jinai kabla ya mtuhumiwa kukamatwa, jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa watu kubambikiziwa kesi.

(a) Kwa vile Jeshi la Polisi ni moja, agizo hilo limewekwa vipi kwa upande wa Zanzibar na utekelezaji wake ukoje.

(b) Je, ni hatua gani zimeshachukuliwa kwa upande wa Zanzibar tokea kutolewa kwa agizo hilo.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

21. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Awamu ya Nane imekuwa ikijitahidi sana kuhimiza usafi wa miji yetu pamoja na usafi wa maeneo katika maeneo mbali mbali ikiwa ni pamoja na jimbo la Nungwi.

(a) Je, ni hatua gani ambazo Serikali imepanga kuzichukua ili kukabiliana na hali hiyo ya uchafu wa mazingira hasa mahotelini.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa maeneo hayo magari ya kuzolea taka.

(c) Kwa kuwa taka hizo hutiwa moto ovyo na moshi wake ni hatari kwa afya ya binadamu, Je, kuna mpango gani wa kujenga sehemu maalum ya kuzichoma taka hizo.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

86. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto:

Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja imeanzisha utaratibu mzuri wa kuangalia wagonjwa kwa kutumia kadi, hata hivyo bado kuna malalamiko na changamoto.

(a) Je, idadi ya watu wawili wanaoruhusiwa kwa wakati mmoja ilizingatia tabia ya jamii zetu.

(b) Ni kwa kiasi gani wananchi wamepewa elimu juu ya utaratibu huo.

(c) Kwa nini kila siku kuna tatizo la foleni kubwa kwenye utoaji wa kadi.

112. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) Atamuuliza Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi sasa dunia nzima imekumbwa na maradhi ya Uviko 19 hivyo kupelekea wananchi kushauriwa kuvaa barakoa kila wanapokuwa kwenye mikusanyiko. Hali hii imepelekea watu kuvuta hewa ya oxygen na kutoa hewa ya carbon dioxide na kuirejesha tena carbon dioxide kuivuta kwa sababu ya kuvaa barakoa.

(a) Je, kuvaa barakoa kwa muda mrefu hakuwezi kusababisha athari kwa afya zetu.

(b) Kwa wananchi ambao wana matatizo ya ugonjwa wa kupumua kama vile pumu. Je, kuvaa barakoa kwa muda mrefu haileti tatizo jengine kiafya.

(c) Je, kuna athari yoyote inayotokana na uvutaji wa hewa kwa baadhi ya barakoa zinazotoka nchi za nje ambazo zina uasili wa vumbi vumbi.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

47. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa juhudi zake za kumaliza ujenzi wa jengo la Terminal III pamoja na barabara ya kwenda kwenye jengo hilo. Hatua ambayo inatarajiwa kuongeza idadi ya ndege kubwa zitakazotua Zanzibar na kuongeza idadi ya watalii.

(a) Kwa kuwa jengo hilo limemaliza ujenzi wake ni lini linatarajiwa kuzinduliwa rasmi.

(b) Kwa kutambua kwamba uwepo wa jengo hilo kutahitajika wafanyakazi wengi na kwa kutambua hilo Mamlaka ya Viwanja vya ndege (ZAA) ilitangaza nafasi za kazi na hatua zote zilifuatwa hata hivyo watuma maombi waliofanikiwa hadi leo hawajaajiriwa. Je, ni nini tatizo lililositisha ajira hiyo.

52. MHESHIMIWA ALI ABDULGHULAM HUSSEIN (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ongezeko la ajali za mara kwa mara katika njia za Jang'ombe skuli kwa wanafunzi ambao wanatumia njia hiyo kwenda Skuli za Jang'ombe msingi na Jang'ombe Sekondari na mpaka sasa hatuoni jitihada za Serikali ya kuondosha tatizo hilo.

Je, Wizara imejipanga vipi kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo ili kupunguza hali hiyo.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

136. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kuboresha na kudhibiti usalama wa maeneo ya skuli za Unguja na Pemba, Serikali imekuwa ikizijengea uzio skuli zake kadiri inavyowezekana. Hata hivyo, skuli ya msingi ya Mjananza imekabiliwa na changamoto mbali mbali zinazozorotesha udhibiti wa eneo lake ikiwa ni pamoja na uwepo wa ujenzi wa nyumba ya familia ya mtu mwenye ulemavu, ujenzi wa nyumba ya kuishi ya mtu binafsi, na umiliki wa sehemu ya ardhi ya mtu binafsi kwenye eneo ambalo lingeweza kuwa sehemu ya uzio wa shule. Kwa kuwa skuli imepata mfadhili wa kujenga uzio kwa ajili ya uhifadhi wa skuli hiyo pindi changamoto hizo zikiondoka.

(a) Je, ni lini Serikali itafidia uhamisho wa ujenzi wa nyumba ya familia ya mtu mwenye ulemavu katika eneo jengine nje ya eneo linalotarajiwa kuwa la uzio wa skuli.

(b) Je, ni lini Serikali itafidia uhamisho wa ujenzi wa nyumba ya kuishi ya mtu binafsi kupelekwa eneo jengine nje ya eneo linalotarajiwa kuwa la uzio wa skuli.

(c) Je, ni lini Serikali itafidia sehemu ya ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi kwenye eneo ambalo lingeweza kuwa sehemu ya uzio wa skuli.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

118. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Wananchi wa Shehia ya Chukwani, Shakani, Mbweni na Michungwani nyumba zao zilizopelekea kuchorwa kwa maandishi ya rangi nyekundu sambamba na kupigwa picha wao wenyewe na kuzuiwa kuendeleza ujenzi wa nyumba zao na shughuli tofauti ikiwemo kilimo.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuzuiliwa kwa ujenzi katika maeneo hayo.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022:**

Ripoti ya Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**18 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**